

# Ripoti ya Haki

# Zilizopotea



**act!onaid**  
tanzania

Ripoti ya

**Haki**

**Zilizopotea**



**act:ona**id  
tanzania





Shirikisho la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (TANGO)  
na Action-aid Tanzania

Shirikisho la Mashirika yasiyo ya Kiserikali (TANGO)  
S.L.P 31147 Dar es Salaam  
Simu: + 255 222744581/2  
Tovuti: [www.tango.or.tz](http://www.tango.or.tz)  
Barua pepe: [tango@bol.co.tz](mailto:tango@bol.co.tz)

@ Action-aid Tanzania na TANGO (2006)

Kimepigwa chapa na Inter Press of Tanzania Limited.

Haki zote zimehifadhiwa

## YALIYOMO

Shukrani.....	v
Utangulizi.....	1
Malengo.....	2
Malengo ya utafiti.....	4
Kupunguza umaskini wa kipato.....	4
Kuhakikisha watoto wote wanapata elimu.....	5
Usawa wa kijinsia.....	7
Kupunguza vifo vya akinamama na watoto.....	8
Mazingira bora.....	10
Changamoto, mapungufu na mapendekezo.....	11
Tuliyojifunza.....	12
Hitimisho.....	13
Ripoti ya takwimu.....	14

## SHUKRANI

TANGO na Action-Aid wanapenda kutoa shukrani kwa mashirika na watu wote walioshiriki katika Utafiti huu.

Kwanza tungependa kutambua mchango wa watafiti kutoka mitandao washirika wa TANGO (District and regional NGO network).

Pili watu wote vijijini walio jibu dodoso na kushiriki katika majadiliano ya vikundi.

### **Orodha ya watu walioshiriki katika utafiti na uandaaji wa repoti**

Laurent Wambura	<b>Afisa katika Action Aid Tanzania</b>
Ngunga Tepani	<b>Mratibu wa mradi</b>
Dr.Charles Sokile	<b>Mtafiti Mkuu</b>
Faustin Mayunga	<b>Mtakwimu</b>
Aloysia Shemdoe	<b>Mtafiti msaidizi</b>
Aileen Chuma	<b>Mtafiti msaidizi</b>
Nestory Masswe	<b>Mtafiti msaidizi</b>
Venance Mlali	<b>Mratibu msaidizi Morogoro</b>
Seraphina Chodota	<b>Mratibu msaidizi Njombe</b>
Essore Maregeri	<b>Mratibu msaidizi Same</b>
Paschal Kilagula	<b>Mratibu msaidizi Tabora</b>
Omar Ame Jecha	<b>Mratibu msaidizi Zanzibar</b>
Maryam Abubakar	<b>Mratibu msaidizi Zanzibar</b>
Zaa Twalangeti	<b>Usanifu</b>



## Utangulizi

### Sura ya nchi

Tanzania ni nchi iliyopo Africa Mashariki, yenye watu milioni 34(sensa ya 2002). Uchumi wake unategemea kilimo, kinachochangia asilimia 50 ya jumla ya pato la nchi kwa mwaka, na asilimia 85 ya mauzo ya nje. Hali ya hewa ya Tanzania inasumbuliwa na ukame na mafuriko. Karibu nusu ya watu wanaishi katika dimbwi la umaskini. Wastani wa kuishi wa mtanzania ni miaka 47.

Umaskini Tanzania unajidhihirisha kwa kuwa na watu wengi wenye vipato vidogo, idadi kubwa ya vifo vinavyotokana na sababu zinazozuilika, lishe hafifu na kutoshiriki kwa wananchi katika maamuzi ya kisera. Umaskini unajidhihirisha zaidi katika maeneo ya vijijini, ambapo asilimia 70 ya watanzania wanategemea zaidi shughuli za kilimo.

Tatizo lingine ni ukosefu wa mipango ya kijamii( social safety nets), ambalo linasababisha watoto wanaotoka kwenye familia maskini kukosa msaada wowote wa kijamii kwa hiyo kujiingiza katika ajira ngumu na wasichana kujihusisha na ukahaba mambo yanayowaweka kwenye mazingira ya kupata maambukizi ya ukimwi.

Pamoja na msisitizo wa usawa wa kijinsia, bado wanawake wengi wanatumia muda wao mwingi katika kazi za uzazi kama kuteka maji, kutafuta kuni, kuhudumia watoto licha ya kushughulikia kazi za uzalishaji.

Pamoja na yaliyoelezwa hapo juu, serikali inaeleza kwamba imeweza kurekebisha na kukuza uchumi. Vielelezo vya mafanikio haya ni kushuka kwa riba na kutoshuka kwa thamani ya shilingi. Kwa upande wa mafanikio katika uchumi mkuu yametokana na serikali Kuelekeza mapato yake kwenye nyanja hii kuliko kuboresha huduma za jamii.

### **Malengo ya Milenia (MDGS)**

Mwaka 2000, nchi 189 wanachama wa Umoja wa Mataifa, ikiwemo serikali ya Tanzania, ziliahidi kuongeza juhudi za makusudi za kupunguza umaskini duniani. Viongozi walitia saina tamko la Milenia (Millennium Declaration) .

Kupitia tamko hilo viongozi wa nchi zote duniani waliahidi kwa dhati kuongeza rasilimali katika elimu, kuhakikisha suala la jinsia linazingatiwa, kupunguza vifo vya watoto waliopo chini ya miaka mitano, Kuboresha hali ya huduma ya afya kwa akina mama, kuongeza juhudi katika mapambano na UKIMWI na kuondoa magonjwa sugu kama malaria, kuhakikisha kwamba hali ya mazingira inaboreshwa na kulindwa. Pamoja na kuboresha ushirikiano wa kimataifa ili kuongeza juhudi za pamoja za kuondoa umaskini.

Tamko la Milenia linazitaka nchi zilizotia sahihi tamko kuchukua hatua za makusudi kutimiza malengo yote nane ya milenia ifikapo mwaka 2015. Tofauti ya tamko la Milenia na matamko mengine ya Umoja wa Mataifa ni kwamba linazingatia kwamba ushiriki wa wadau mbalimbali ni muhimu kwa kufanikisha Malengo hayo.

Pamoja na mashaka kwamba malengo ya milenia ni mkusanyo wa matamko yaliyopita na kwamba hayatimiziki, au hayataweza kuleta mafanikio yenye mabadiliko ya kishindo, vyama na makundi ya kiraia na kijamii nchini Tanzania hata ya

kimataifa wanaimani kwamba malengo ya milenia yanaweza kutumika kama

nyenzo ya kupima na kuhimiza uwajibikaji wa serikali na wabia wengine (nchi tajiri) katika jitihada za kupunguza umaskini na kufikia maendeleo endelevu.

Nchini Tanzania harakati za kuhimiza utekelezaji wa malengo ya milenia zilianza na warsha ya wawakilishi wa vyama na vikundi vya kiraia iliofanyika katika hoteli ya Peacock tarehe 28 na 29 Juni mwaka 2004.

Mkutano huu ulitanguliwa na jitihada za SAHRINGON<sup>1</sup> juu ya tathmini ya utekelezaji wa malengo ya Milenia na pia, NGO Policy Forum (NPF) na Feminist Activism Coalition (Femact) juu ya kufuatilia utekelezaji wa mikakati ya kupunguza umaskini nchini.

Baada ya mwaka mmoja mashirika yaliyotajwa hapo juu na mengine kwa kushirikiana na muungano wa mashirika yasiyo ya kiserikali (TANGO) na jamii ya kiraia yaliunda mtandao wa malengo ya milenia Tanzania (Tanzania Global Call to Action Against Poverty Coalition).

Lengo kuu la kampeni ya malengo ya milenia Tanzania ni kushinikiza serikali ya Tanzania na wadau wengine katika kutekeleza na kufikia malengo ya milenia nchini Tanzania. Mwaka 2005 ni mwaka wa kutathmini jinsi ambayo serikali mbalimbali duniani zimetokeleza malengo ya milenia, katika miaka mitano ya mwanzo.

Viongozi wa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa walikutana na kutathmini utekelezaji wa malengo ya milenia na kupanga upya mipango ya kufanikisha malengo ya milenia. Katika mkutano wa dunia kuhusu malengo ya milenia uliofanyika Septemba 2005 wanachama walitoa ripoti zao kuhusu utekelezaji wa malengo ya milenia.

Utafiti huu unalenga kupata na kutoa maoni ya wananchi hasa watu maskini vijijini kuhusu utekelezaji wa malengo ya milenia na mikakati ya kupunguza umaskini nchini Tan-





Ripoti ya utafiti huu itatoa mtazamo wa wananchi kuhusu utekelezaji wa malengo ya milenia ambao utalinganishwa na ripoti ya serikali.

### **Malengo ya utafiti**

Lengo kuu la utafiti lilikuwa kukusanya mawazo ya watu maskini kuhusu utekelezaji wa malengo ya milenia. Utafiti huu ni sehemu ya mradi wa kimataifa wa Action-Aid unaoitwa "Haki zilizopotea". Mradi huu unalenga kutoa mawazo ya wananchi kuhusu utekelezaji wa malengo ya milenia.

### **Matokeo**

Yafuatayo ni maelezo kuhusu matokeo ya utafiti. Pamoja na ripoti ya serikali kuhusu utekelezaji wa malengo ya milenia iliyotolewa katika mkutano wa Umoja wa Mataifa juu ya utekelezaji wa malengo ya milenia kwa miaka mitano ya mwanzo mawazo ya wananchi ni kama ilivyoelezwa hapo chini.

Matokeo ya utafiti yatafuata mtiririko wa namna malengo yalivyoorodheshwa katika tamko la Milenia.

### ***Lengo # 1: Kupunguza umaskini wa kipato uliokithiri na ukosefu wa chakula.***

Katika lengo hili utafiti ulishughulika zaidi na umaskini wa kipato na ukosefu wa chakula, kuliko masuala ya kiuchumi yaliyofafanuliwa zaidi kwenye lengo nambari 8.

Washiriki kutoka asilimia 94.0 ya vijiji vilivyotafitiwa walikiri kuwepo kwa familia zilizo katika umaskini wa kupindukia. Tokeo la muhimu ni kwamba ni watu wachache sana katika vijiji vilivyohusishwa katika utafiti wanaweza kupata milo mitatu kwa siku, wengi wanaweza kupata mlo mmoja tu kwa siku. Kuna sehemu ambazo wazee na watu wenye ulemavu wanashidwa kupata hata mlo mmoja kwa siku.

Kwa mfano katika kijiji cha Nyakasanga, wilayani Kibondo, kati ya vifo 344 vilivyotokea mwaka uliopita, asilimia 54.9 sawa na vifo 189 vilitokana na sababu za njaa na ukosefu wa chakula. Kati ya watu 324 waliohojiwa, asilimia 91.8 walikubali kwamba wamewahi kukumbwa na tatizo la kutunza mazao ya chakula baada ya kuvuna. Hali mbaya zaidi ni kwamba familia nyingine kutokana na ukosefu wa ardhi hupata kilo 20 tu za nafaka kwa mwaka.

Kwa sababu ya njaa iliyokithiri baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Masasi huhamama ili kutafuta chakula. Mfano ni kijiji cha Tuli kilichokuwa na familia 500 lakini kwa sasa kina familia 150 tu. Wakazi wengi wa vijiji vilivyo husika katika utafiti walisema kwamba wanaishi kwa chini ya shilingi 500 (ambazo ni senti 50 za Kimarekani) kwa siku.

Hali ya wanawake katika maeneo yaliyohusika kwenye utafiti yanaonyesha kwamba wanawake ndio wanaochangia zaidi kipato cha familia kwa kufanya kazi ngumu kwa zaidi ya masaa 16 kwa siku, maeneo hayo ni Same, Kilosa na Njombe.

Kwa upande wa Zanzibar hasa kisiwa cha Pemba ukosefu wa chakula bora umesababisha kuwepo kwa watu wengi wenye utapiamlo. Wakazi wengi wa vijiji vilivyohusika kwenye utafiti wana utapiamlo. Vifo vinavyotokana na njaa vilitokea katika wilaya za Kiuyu – Mbuyuni na Micheweni.

Tatizo hili linazidishwa na serikali kutotoa pembejeo za kilimo kwa wananchi.

### ***Lengol # 2: Kuhakikisha watoto wote wanapata elimu ya msingi.***

Katika vijiji 357 vilivyohusika kwenye utafiti asilimia 96.1 vilikuwa na shule. Katika sehemu ambazo hazina shule, shule zilizokaribu zipo umbali wa kilomita tatu kutoka kijijini.

Ingawa uandikishaji wa watoto katika shule za msingi umefikia asilimia 100, wazazi 345 kati ya waliohojiwa, yaani asilimia 64.1, hawajaridhika na ubora wa elimu inayotolewa. Kwenye kijiji kimoja kilichofanyiwa utafiti hakuna hata mwanafunzi





mmoja wakike aliye chaguliwa kwenda sekondari tangu mwaka 1975.

Wakazi wa vijiji viliyohusika katika utafiti walisema kwamba watoto wanaotoka kwenye familia maskini wanashindwa kulipa michango ya ada.

Tatizo lingine ni kwamba hali ya maisha ya walimu ni mbaya, kiasi cha walimu kukosa ari ya kazi. Walimu wengi hawajapata mafunzo zaidi baada ya kuanza kazi kiasi cha miaka kumi iliyopita. Wengine hawajapandishwa vyeo kwa miaka mingi.

Shule nyingi hazina nyumba za walimu. Tatizo hili linasababisha walimu watembe umbali mrefu kwenda shuleni.

Shule nyingi bado zinatumia mtindo wa uchapaji viboko wanafunzi. Pamoja na viboko kuna aina nyingine za adhabu zinazotolewa kwa mfano shule ya msingi Michenga, wilaya ya Ruangwa, wanafunzi wanaoshindwa mitihani wanaambiwa kwenda porini kuokota kuni. Kwa mfano mwanafuzi akipata asilimia 60 anaambiwa kwenda kuokota kuni 40 kama fidia ya maksi alizokosa.

Unyanyasaji na ndoa za umri mdogo, mimba na uchangiaji wa ada ya shule vinasababisha watoto wengi kuacha shule.

Shule nyingi hazina walimu wa kutosha, vitabu na madawati na zana nyingine za kufundishia. Katika shule nyingi zilizohusika katika utafiti kuna uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi wanne, tatizo hili linasababisha wanafunzi wasifanye vizuri katika masomo yao.

Pamoja na matatizo haya, mpango ya MEM umesaidia wanafunzi waliokosa shule kupata nafasi nyingine ya kusoma.

Pamoja na matatizo ya ukosefu wa shule, tatizo la udini linasababisha watoto wengi katika sehemu mbali mbali

za Tanzania kukosa shule. Mfano ni kwenye vijiji vyenye shule zilizojengwa na makanisa, ambapo Waislamu hawataki kupeleka watoto wao kwa kuogopa kwamba watafundishwa maadili ya Kikristo.

### **Lengo # 3: Usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake**

Katika shule 352 zilizo husika kwenye utafiti huu shule 299 ambazo ni asilimia 84.9 zina vyoo vya wasichana na wavulana. Shule 53 ambazo ni asilimia 15.1 hazikuwa na vyoo vya wanawake.


Katika vijiji 353 vilivyohusika katika utafiti waliohojiwa walisema kwamba asilimia 74.5 ya watoto wa kike vijijini mwao hawaendi shuleni kwa sababu ya matatizo yaliyoainishwa hapo juu.

Katika vijiji vingi wanawake bado hawawezi kuongea mbele ya wanaume, kwa ujumla wanakandamizwa na wanaume. Mara nyingi na kwenye sehemu nyingi zilizotembelewa na watafiti, wanawake hawashiriki katika vikao vya kutoa maamuzi kuhusu maisha yao na watoto.

Wakiwa ni watafutaji wa chakula katika familia maskini, wanawake wanafanya kazi kwa muda mrefu na kupewa kipato kidogo. Hata hicho kidogo kinachukuliwa na kutumiwa na wanaume. Utafiti umebaini kwamba wanawake wanapata kipato kidogo kuliko wanaume. Matokeo haya yalidhihirishwa na jibu la swali lililoulizwa kama kuna tofauti ya vipato kati ya wanawake na wanaume kwenye vijiji vilivyohusika kwenye utafiti. Asilimia 67.3 walikubali kwamba wanawake vijijini mwao wanapata vipato vidogo ikilinganishwa na wanaume.

Kuhusu suala la mikopo asilimia 95.1 ya waliohojiwa walisema kwamba ni vigumu sana kupata mikopo hata ruzuku kutoka serikalini, hasa kwa wanawake ambao wengi wao hawana elimu, ardhi na hawaelewi haki zao.





Kama ilivyoielezwa hapo juu utafiti uliangalia hata suala la umiliki wa ardhi kwa wanawake na iligundulika kwamba kwa ujumla wanawake katika maeneo yaliyo husika kwenye utafiti hawa miliki aridhi.

**Malengo # 4, 5, 6 Kupunguza vifo vya watoto na akinamama vinavyotokana na kujifungua na kupambana na magonjwa kama Malaria, Kifua Kikuu na virusi vya UKIMWI.**

Watafiti waliona kwamba kupata majibu kamilifu kuhusu malengo yanayohusu afya, ambayo ni malengo nambari 4, 5 na 6 ni vizuri wakauliza maswali kwa pamoja.

Kwa ujumla vituo vya afya vipo umbali mrefu kutoka vijijini. (vya karibu zaidi vipo umbali wa kilometa 5), lingine ni kwamba vituo vingi havina wauguzi na vifaa vya kutendea kazi.

Katika maeneo mengi wauguzi ndiyo wanaofanya kazi za kidaktari pia. Kwa ujumla vijiji vingi havina zahanati au vituo vya afya.

Utafiti huu ulibaini kwamba kuna tatizo lingine ambalo ni ukosefu wa dawa na kuwa ingawa maduka ya dawa ya binafsi yapo, bei ya dawa ni kubwa sana kiasi kwamba watu wengi wanashindwa kununua dawa zinazouzwa kwenye maduka hayo.

Ingawa kuna jitihada za kuhakikisha kwamba akinamana wajawazito wanapata huduma karibu na nyumbani, bado wanawake wengi wanapata huduma kutoka kwa wakunga wa jadi. Katika vijiji vingi kulikuwepo na matukio ya kina mama kufariki kabla ya kupata huduma, kutokana na umbali wa vituo vya afya na upungufu wa zana za kazi kwenye vituo vingi.

Katika maeneo mengi vifo vya watoto vinatokea mara kwa mara, wengi wanakufa kwa sababu ya magonjwa yanayotibika kama vile malaria. Ingawa tafiti nyingine zinaeleza kwamba UKIMWI ndiyo chanzo kikubwa cha vifo nchini Tanzania, ni katika sehemu chache ambapo watu walizungumzia suala hilo. (Hata katika ofisi za vijiji hazikuwepo taarifa au takwimu kuhusu UKIMWI).

Kwa ujumla wananchi hawako tayari kwenda kupima. Hata bila taarifa rasmi kuhusu ukimwi, kutokana na mahojiano, utafiti ulibaini kwamba Tanzania Bara ina watu wengi walioathirika na UKIMWI kuliko Zanzibar, tofauti hii inatokana na utofauti wa tabia za watu wa bara na wale wa Zanzibar.

Kwa ujumla wananchi wengi vijijini hawana uelewa wa kutosha kuhusu UKIMWI jambo linalosababisha wasioanishe vifo hivyo na UKIMWI. Mfano ni katika kijiji cha Tandahimba ambapo mnamo mwaka 2004, kati ya watu 10 wanaume 2 na wanawake 3 waliohudhuria vituo vya afya walingudulika kuwa na Virusi vinavyo sababisha Ukimwi, lakini tofauti na mjini ambapo wanaoishi na virusi vya UKIMWI wananyanyapaliwa, katika kijiji hiki watu hawa hawakunyanyapaliwa kutokana na watu kutoelewa jinsi gani Ukimwi unavyoambukizwa.

Waliohojiwa walisema kwamba mara nyingi madaktari hawatoi taarifa kamili kuhusu vifo vinavyotokana na Ukimwi, wanataja ule ugonjwa wa mwisho aliokuwa nao mgonjwa kabla ya kufa, watu hawaelezwi kwamba ugonjwa huo umesababishwa na upungufu wa kinga mwilini. Wanavijiji wengi walisema kwamba Malaria ndiyo chanzo kikubwa cha vifo.

Sababu ikiwa kwamba watu wengi ni maskini sana kiasi cha kushidwa kununua vyandarua vyenye dawa za kuangamiza mbu. Tatizo lingine ni la bei kubwa ya uchunguzi wa daktari, hali hii inasababisha watu kununua dawa moja kwa moja bila kumuona daktari. Tatizo hili limesababisha wananchi wengi waliohojiwa kuwa na miili sugu kwa dawa nyingi za malaria.



### **Lengo # 7: Kuwepo kwa mazingira bora, salama na endelevu**

Utafiti ulilenga masuala ya upandaji na ukataji miti, ulindaji wa vyanzo vya maji na usafi wa mazingira ya jamii kwa ujumla.

Ukataji miti kwa ajili ya biashara unaathiri mazingira ya sehemu nyingi, utafiti ulibaini tatizo hili hasa katika wilaya ya Masasi.

Kuhusu upatikanaji wa maji waliohojiwa walisema kwamba karibu kila mahali kuna vyanzo vya maji lakini tatizo ni umbali ambao watu hasa wanawake wanatembea kuyapata. Pia tatizo la usalama wa maji hayo.

Kwa wastani wanatembea maili 7 ili kupata ndoo moja ya ujazo wa lita 20.

Shule nyingi hazina maji, kwa mfano huko Kigoma kunasemekana kulitokea tukio la wanafunzi wa shule moja kumnyang'anya mama mmoja ndoo ya maji, aliyoyapata umbali wa Kilomita 3. Sehemu nyingine ambapo kuna matatizo ya maji ni kijiji cha Tuli kilichopo nje kidogo kutoka manispaa ya Tabora. Katika kijiji hiki chanzo pekee cha maji ni madimbwi ya maji yanayotokana na mvua. Maji yanatumika na watu na wayama kwa pamoja. Wakati wa kiangazi watu na wanyama wanatembea umbali wa kilomita 15 kupata ndoo moja ya maji.

Nyumba nyingi zilizotembelewa zilielezwa kwa nyasi, kwa hiyo katika sehemu zenye matatizo na majanga kama vile vimbunga au mvua kali, nyumba hizi zinashidwa kuhimili majanga haya kwa hiyo zinabomoka na kuua watu. Aina ya vyoo ambavyo vinatumika kwa wingi katika maeneo yaliyotembelewa ni vyoo vya shimo (Pit-latrines).

### **Lengo # 8: Kuendeleza mahusiano ya kimataifa kwa ajili ya maendeleo endelevu**

Katika kipengele hiki utafiti ulilenga kuelewa namna masuala ya haki za binadamu, utawala bora na uwajibikaji wa viongozi yanavyochukuliwa katika maeneo husika.

Kulikuwepo na visa vya unyanyasaji wa watu, kupitia mahakama za kienyeji katika baadhi ya vijiji vilivyotembelewa.

Katika maeneo mengine kulikuwepo na matumizi mabaya ya michango ya wakulima, kwa mfano huko Tandahimba katika msimu wa mwaka 2004/2005 serikali ya wilaya ilichangisha jumla ya milioni 472 kwa ajili ya kununua pembejeo za zao la korosho, lakini ni milioni 408 tu zilizotumika katika kununulia pembejeo, kitendo hiki kilisababisha wakulima wapatao 314 kukosa pembejeo ingawa walichanga pesa. Hadi wakati wa utafiti walikuwa hawajarudishiwa pesa zao au kupewa msaada wowote

Lingine lililojitokeza ni kwamba mahakamani, wafanyakazi na nyenzo za kutimiza haki havitoshi, kiasi cha kupelekea kuwapo kwa rushwa katika mfumo wa sheria katika maeneo yaliyotembelewa. Katika kijiji cha Maha wilayani Tandahimba wafanyakazi wa mahakama waliomba walalamikaji kutoa gharama za matunzo ya walalamikiwa hadi hapo kesi zao zilipoamliwa.

Tatizo lingine ni ugomvi kati ya wakulima na wafugaji, mfamo ni maeneo ya Same na Kilosa ambako kuna matukio ya mapigano ya wakulima na wafugaji lakini serikali haijapata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo linalopoteza maisha ya watu katika maeneo husika.

Waliohojiwa walisema suala lingine linalowatatiza ni kutofaidika na uwekezaji wa rasilimali zinazopatikana katika maeneo yao. Wanasema kwa kiwango kikubwa ni serikali kuu inayonufaika na mapato yanayopatikana ( mfano dhahiri ni huko Pemba ambapo wananchi waliondolewa katika makazi yao ya kudumu ili kupisha ujenzi wa mradi wa uwekezaji, lakini hawakupewa fidia yoyote).

Kuhusu utawala, bado maagizo yanatoka juu kwenda chini, wananchi hawashiriki katika kufanya maamuzi, na la zaidi ni kwamba viongozi katika ngazi ya serikali za mitaa wanakosa mbinu za utawala shirikishi.

### **Changamoto, mapungufu, mafunzo na mapendekezo**

Changamoto kuu katika utafiti huu zilikuwa ni muda mfupi uliotolewa na wafadhili na lingine lilikuwa ni matatizo ya usafiri na mawasiliano wakati watafiti walipokuwa vijijini.

Matatizo yalioelezwa hapo juu yaliambatana na tatizo la kutotosha kwa pesa za kuendesha utafiti huu kikamilifu.







### **Yafuatayo ni mambo tuliyojifunza:**

- Wakusanyaji wa taarifa hawakuwa na uelewa wakutosha kuhusu masuala ya Malengo ya Milenia.
- Muundo wa dodoso haukuruhusu vya kutosha uibuaji wa masuala mengine, kwa mfano, haikutoa mwanya kudodosa habari zinazohusu shughuri za kilimo, mifugo, uchimbaji wa madini na utalii.
- Baadhi ya taarifa zilizotolewa zilikuwa zimepitwa na wakati.
- Baadhi ya watu waliohojiwa walitaka wapewe pesa kwa kujibu dodoso.

### **Mapendekezo yanayotokana na utafiti huu:**

- Utafiti urudiwe na upewe rasilimali zaidi ili ufanyike nchi nzima
- Serikali isiache kazi yake ya kutoa huduma bora za jamii kwa watanzania wote.
- Kuna haja ya kutolewa kwa Elimu zaidi ya kiraia kuhusu haki za kiraia, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) na malengo ya milenia katika ngazi za vijiji.
- Sera ya Ukimwi ipitiwe upya ili iweke mazingira yatakayowafanya wanaoishi na virusi vya UKIMWI kuwa wazi na kuishi kwa matumaini zaidi.
- Uchangiaji wa gharama za afya na elimu ufutwe kabisa, kwa sababu wananchi wengi hawawezi kumudu.
- Serikali iboreshe huduma za elimu na afya katika
- Serikali iboreshe huduma za elimu na afya katika ngazi zote kwa kuongeza wataalam, dawa na nyenzo.
- Serikali ibuni mbinu za kuhakikisha kwamba wananchi vijijini wanaweza kuepukana na tatizo la umaskini wa kipato.

## HITIMISHO

Ingawa serikali ya Muungano na ile ya Zanzibar zimechukua hatua mbali mbali za kupunguza umaskini kama ilivyoielezwa katika MKUKUTA na MKUZA, bado kuna kazi kubwa ya kufanya ili kufikia malengo ya milenia ifikapo 2015.

Utafiti umeonyesha kwamba ingawa serikali inajivunia kupanda kwa uchumi, wananchi vijijini hawajanufaika sana na matunda ya ukuaji wa uchumi, msamaha wa madeni na uwekezaji.

Ili kutimiza malengo ya milenia ifikapo mwaka 2015 tunahitaji serikali kufuata ahadi na kuacha kuvunja ahadi ilizozitoa kwenye Tamko la Milenia.

Kwa upande wa wahisani, na wabia wa maendeleo wengine, pendekezo ni kuwa, waongeze ubora na thamani ya misaada wanayotoa kwa nchi maskini. Hili liambatane na kuwepo kwa haki na usawa wa kibiashara na ufutaji wa madeni, ili nchi maskini ziwekeze kwenye maeneo muhinu kama afya, elimu na uboreshaji wa miundo mbinu.

Kwa hiyo, kinachohitajika siyo tu kuelezea ukuaji wa uchumi kitakwimu, wakati maisha ya wananchi yanaendelea kudidimia katika lindi la umaskini, kiasi kwamba wanakosa hata huduma za msingi za kijamii kama vile afya bora, elimu na stadiza kumudu maisha.

Serikali haina budi kuchukulia ripoti hii kwa uzito unaostahili kwa sababu maelezo yaliyomo ni maoni na vilio vya wananchi kutoka katika wilaya 14 za Tanzania Bara na Visiwani.

Tuna imani kwamba maoni na vilio hivi vitatufanya tuelekeze nguvu zaidi katika kupambana na umaskini wa kupindukia, njaa na vifo vinavyotokana na vyanzo vinavyoweza kuzuilika na magonjwa yanayoweza kutibika. Inawezekana kila mtu akitimiza wajibu wake ipasavyo.



**RIPOTI YA TAKWIMU**

- Q1. Kati ya vijiji 357, vijiji 343 ambayo ni asilimia 96.1 vinashule. Vijiji 14 ambavyo ni asilimia 3.9 havina shule.
- Q2. Kati ya vijiji 355, vijiji 297 ambavyo ni asilimia 83.7 havina shule za sekondari, ni asilimia 16.1 tu ya vijiji vyenye sekondari.
- Q3. Kati ya vijiji ambavyo havina shule, shule za karibu zipo umbali wa kilometa 3, lakini kwenye vijiji asilimia 8.8 ambayo ni vijiji 25, shule zipo umbali wa zaidi ya kilometa 3 kutoka kijijini.
- Q4. Kati ya shule 352, shule 299 ambazo ni asilimia 84.9 zilikuwa na vyoo vya wasichana, na shule 53 ambazo ni asilimia 15.1 hazikuwa na vyoo kwaajili ya wasichana.
- Q5. Kati ya wazazi 345 waliohojiwa, 221 ambao ni asilimia 64.1 hawakuridhika na ubora wa elimu inayotolewa katika shule zilizopo karibu na vijiji hivyo
- Q6. Utafiti ulibaini kwamba katika vijiji 348, kwa ujumla idadi ya walimu kwa ilikuwa 101. Hata hivyo asilimia 29.0 hawadhurii darasani mara kwa mara.
- Q6a. Kati ya watu 346 waliohojiwa, watu 229 ambao ni asilimia 66.2 hawakuridhika na ubora wa huduma inayotolewa na shule zilizopo karibu nao.
- Q6b. Kati ya shule 347, shule 307.2 ambazo ni asilimia 88.8 hazikuwa na mpango wa chakula kwa wanafunzi.
- Q7. Asilimia 93.8 ya watu waliohojiwa walisema kwamba shule ya msingi ni bure.
- Q8. Asilimia 6.2 ya waliohojiwa hawawezi kumudu gharama za shule.

- Q9. Kati ya wanafunzi 353 wa kike asilimia 74.5 hawaendi shule.
- Q10. Kati ya vijiji 354, vijiji 237 ambayo ni asilimia 66.9 havina huduma ya afya ya msingi (primary health care services).
- Q11. Kati ya vijiji 303 ambavyo havina huduma za afya ya msingi, vijiji 225 ambavyo ni asilimia 74.3 wakazi wake hutembea kilometa 3 kupata huduma za afya.
- Q12. Kati ya madaktari 324 waliopo katika zahanati ni madaktari 197 tu waliokuwa na ustadi wa kazi yao.
- Q13. Kati ya wauguzi 327 ni wauguzi 165 tu ambao ni asilimia 50.5 ambao walikuwa na stadi ya uuguzi.
- Q14. Kati ya wagongwa 294, ni wagonjwa 243 ambao ni asilimia 82.7 wanaopata matibabu katika hospitali za umma, asilimia 17.8 wanapata matibabu kwenye vituo vya afya binafsi.
- Q15. Kati ya watu 341, watu 250 ambao ni asilimia 73.3 walisema kwamba wanalipa pesa ili kupata huduma ya afya/matibabu.
- Q16. Kati ya watu 286 waliohojowa, watu 142 ambao ni asilimia 49.7 hawawezi kumudu gharama za matibabu/ afya.
- Q17. Asilimia 44.1 ya waliohojiwa walisema kwamba hakuna dawa za kutosha katika zahanati.
- Q18. Kati ya watu 334 waliohojiwa, watu 224 ambao ni asilimia 67.1 walisema kwamba vituo vya huduma za afya vya umma vinashidwa kutoa huduma za kutosha.
- Q19. Kati ya waliohojiwa 332, watu 312 ambao ni asilimia 94.0 walisema kuwa vituo vya afya vilivyopo haviwezi kutatua matatizo waliyonayo kutokana na ukosefu wa wataalam.



- Q20. Kati ya wanawake 338 waliohojiwa, wanawake 120 ambao ni asilimia 35.5 walisema kuwa vituo vya afya hukidhi mahitaji yao ya huduma ya afya kabla na baada ya kujifungua.
- Q21. Kati ya watu 349 waliohojiwa, watu 147 ambao ni asilimia 42.1 walisema hakuna mafunzo yanayotolewa kwa ajili ya wakunga.
- Q22. Kati ya vijijji 352 vilivyotafitiwa, vijijji 201 ambavyo ni 57.1, vilikiri kutokea kwa vifo vya wakinamama wakati wa kujifungua miaka ya nyuma.
- Q23. Kati ya vijiji 351 vilivyotafitiwa, vijiji 297 ambavyo ni asilimia 84.6 vilikiri kutokea kwa vifo vya watoto wachanga mwaka uliopita.
- Q24. Kati ya vijiji 353 vilivyotafitiwa, vijiji 231 ambavyo ni asilimia 65.4 vilikiri kuwa na maji ya kunywa ya kutosha.
- Q25. Kati ya watu 345 waliohojiwa, watu 84 ambao ni asilimia 24.3 utembea zaidi ya kilomita tatu kutafuta maji, watu 79 ambao ni 22.9 utembea chini ya nusu kilomita kutafuta maji, na watu 10 ambao ni asilimia 2.9, upata maji nje kidogo ya makazi yao.
- Q26. Kati ya wanavijiji 355, wanavijiji 332, ambao ni asilimia 93.5, walisema kwamba hawajawahi kupata kipato cha Tsh 48,000 ambayo ni wastani wa kipato cha kaya kwa mwezi kilicho wekwa na serikali.
- Q27. Kati ya wanaume 334 wanaume 168 ambao ni asilimia 50.3 wanafanya kazi za kujiajiri na wanafanya kazi siku 20 hadi 25 kwa mwezi.
- Q28. Kati ya wanawake 305, wanawake 155 ambao ni asilimia 50.8 wanafanya kazi siku 25 lakini wanapata kipato kilicho chini ya kile cha serikali.
- Q29. Kati ya vifo 344, asilimia 54.9 ya vifo vinasababishwa na matatizo ya ukosefu wa chakula.

- Q30. Kati ya watu 352 waliohojiwa, watu 324 ambao ni asilimia 91.8 walisema wamewahi kukumbwa na baa la njaa.
- Q31. Kati ya watu 349 watu 328 ambao ni asilimia 94.0 ya waliohojiwa walisema kuna familia ambazo ni maskini wakitupwa.
- Q32. Asilimia 64.6 ya watu waliohojiwa walisema kwamba kuna miezi katika mwaka ambapo wanakosa chakula, kwa hiyo hufanyakazi mbali mbali na kulipwa chakula.
- Q33. Asilimia 97.5 ya waliohojiwa walisema mpango wa chakula wa serikali haukidhi mahitaji ya wananchi.
- Q34. Asilimia 55.7 ya watu waliohojiwa walisema kwamba katika maeneo yao vipato vya wanawake na wanaume haviko sawa.
- Q35. Kati ya watu 156 ambao ni asilimia 67.3 ya watu waliohojiwa kuhusu suala la vipato walisema kwamba katika maeneo yao wanawake wanapata vipato vidogo kuliko wanaume.
- Q36. Asilimia 52.9 ya watoto waliohojiwa katika utafiti wanafanya kazi za kulipwa (child labour).
- Q37. Asilimia 95.1 ya wafanya biashara wanawake walisema hawajapata mikopo yoyote kutoka mabanki au serikali.
- Q38. Ni asilimia 43.1 tu ya wanawake wanamiliki ardhi.



